# Azimio la Beijing:

## Maendeleo na yale ambayo Hayajakamilika katika Kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake

Mtazamo wa kina wa historia na mageuzi ya jukwaa la kuchukua hatua la Beijing katika eneo muhimu la Ukatili Dhidi ya Wanawake.

# Mkutano wa Beijing: Hatua muhimu kuelekea upatikanaji wa Haki za Wanawake

- *Mkutano wa Nne wa Dunia wa Wanawake wa 1995 ulifanyika* Beijing mwaka wa **1995.** Mkutano huu uliwakutanisha kwa pamoja serikali 189 na wanaharakati **17,000.**

- *Mkutano huo uliwezesha kuundwa kwa jukwaa la kuchukua hatua* la Beijing, na ajenda ya msingi ya haki za wanawake katika ngazi ya kimataifa.

**Miaka 30 baadaye, jukwaa la kuchukua hatua linabaki kuwa mojawapo ya maandiko ya msingi katika vuguvugu la kutetea haki za kijinsia.**

# Mpango wa Kimataifa wa Haki za Wanawake Duniani

Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing ni mfumo wa kina na wa kimkakati ambao unalenga kuendeleza haki za wanawake katika nyanja zote za maisha, unaobainisha maeneo muhimu 12 :

| | |
|---|---|
| **1.** Elimu na Mafunzo kwa Wanawake | **2.** Mamlaka na kutoa maamuzi |
| **3.** Wanawake & Afya | **4.** Mifumo ya Taasisi katika Maendeleo ya Wanawake |
| **5.** Ukatili Dhidi ya Wanawake | **6.** Haki za Wanawake |
| **7.** Wanawake &Kuzuia migogoro na vita | **8.** Upatikanaji wa Taarifa na Vyombo vya Habari |
| **9.** Wanawake & Kupunguza Umaskini | **10.** Mazingira |
| **11.** Wanawake na Uchumi | **12.** Mtoto wa Kike |

Kila eneo lina lengo maalum na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa na serikali, mashirika ya kimataifa na mashirika ya kiraia ili kufikia usawa wa kijinsia. Tume ya Umoja wa Mataifa ya Hali ya Wanawake ni chombo cha kimataifa cha uwajibikaji ambacho serikali zinapaswa kutoa taarifa kuhusu maendeleo yao katika utekelezaji.

Kila baada ya miaka 5, kumekuwa na mapitio ya maendeleo ya maazimio yaliyofanywa Beijing ambayo yanaleta uelewa mapya na vipaumbele.

# Kukomesha Ukatili dhidi ya Wanawake: Ni suala la Msingi la Kuzingatia

Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing linahimiza serikali zichukue hatua kuzuia, kuchunguza na kutoa adhabu kwa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake, kutenda Ukatili Dhidi ya Wanawake ni ukiukwaji wa haki za binadamu pia nikikwazo katika kufikia usawa wa kijinsia.

**Ukatili dhidi ya wanawake unatafsiriwa kama:**

"kitendo chochote cha ukatili wa kijinsia ambacho kinasababisha, au kinachoweza kusababisha madhara ya kimwili, kingono au kisaikolojia au mateso kwa wanawake, ikiwa pamoja na vitisho vitokanavyo na vitendo hivyo, kulazimishwa au kunyimwa uhuru, iwe inatokea katika maisha kwa njia ya uwazi au ya faragha. ."

Kwa nyongeza, Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing linasema "Ukatili dhidi ya wanawake ni udhihirisho wa uhusiano wa kihistoria unaosababisha kutokuwepo na usawa wa mamlaka kati ya wanaume na wanawake, ambao unasababisha kutawaliwa na ubaguzi dhidi ya wanawake unaofanywa na wanaume na kuzuia maendeleo kamilifu ya wanawake."

Kitita hiki ni rejea kwaajili ya aina mahususi za ukatili kama vile: ukatili wa majumbani, ukatili wa kingono, biashara haramu ya binadamu, kufungwa kizazi kwa lazima na kutoa mimba kwa lazima, mauaji ya watoto wakike wachanga na ukeketaji.

# Mikakati Muhimu ya Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing ya Kushughulikia suala la Ukatili Dhidi ya Wanawake

**Kuna malengo3 ya kimkakati yaliyofafanuliwa katika Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing:**

## D.1 Kuchukua hatua jumuishi za kuzuia na kukomesha ukatili dhidi ya wanawake

- Serikali lazima zilaani suala la ukatili, zitunge/ziimarishe mifumo ya kisheria ya Ukatili Dhidi ya Wanawake,ziridhie kanuni za haki za binadamu, zihuishe masuala ya jinsia, ziweke mifumo inayozingatia haki za waathirika, ikiwa ni miongoni mwa mambo mengine.
- Serikali, mashirika ya kijamii, mashirika yasiyo ya kiserikali, sekta za umma & binafsi zinalazimika kutoa huduma zinazopata ufadhili wa kutosha, kwa kutumia lugha mbalimbali na huduma za usaidizi zinazotolewa kulingana na utamaduni wa sehemu husika, kufadhili kampeni za kutoa taarifa kwa jamii ili kukabiliana na kuzuia UWAKI, ikiwa ni miongoni mwa mambo mengine.
- Serikali, waajiri, vyama vya wafanyakazi, jumuiya na mashirika ya vijana, na AZAKI zitokomeze unyanyasaji wa kingono na Ukatili Dhidi ya Wanawake katika taasisi & maeneo ya kazi, wawe na programu za kusaidia wasichana, vijana na wanawake vijana, na kuchukua hatua maalum kwa walio hatarini zaidi ikiwa ni pamoja na wanawake vijana, wanawake waliouhamishoni., wanawake wenye ulemavu, ikiwa ni miongoni mwa wengine

**D.2 Kuchunguza sababu na matokeo ya Ukatili Dhidi ya Wanawake na hatua za kuzuia zenye ufanisi**

- Serikali zinapaswa kuendeleza utafiti na ukusanyaji wa takwimu, kushirikisha matokeo ya utafiti, na kuhimiza vyombo vya habari kuchunguza dhana potofu za kijinsia.

**D.3 Kutokomeza usafirishaji haramu wa wanawake na kusaidia wahanga wa ukatili kutokana na ukahaba na usafirishaji haramu wa binadamu**

- Serikali za nchi husika, wasafirishaji na wapokeaji, mashirika ya kikanda na kimataifa yanapaswa kuridhia mikataba ya kimataifa kuhusu utumwa na usafirishaji haramu wa binadamu, kushughulikia mambo ya msingi yanayo sababisha usafirishaji haramu wa binadamu, kuratibu hatua kati ya mamlaka na taasisi zinazotekeleza sheria, na kuandaa programu za mafunzo ya kuzuia ukatili wa kingono na usafirishaji haramu wa binadamu.



# Maendeleo na Mapungufu Katika kipindi cha Miaka 30 Iliyopita

## Beijing + 5 (2000): Kuthibitisha Maazimio, Kutambua Mapungufu

- **Mafanikio:** Kuthibitisha tena dhamira ya kimataifa ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake, kuongeza umakini kwenye Ukatili Dhidi ya Wanawake kama suala la usawa wa kijinsia.
- **Changamoto:** ukosefu wa utekelezaji, ukusanyaji duni wa takwimu
- **Mahitaji muhimu:** ukusanyaji bora wa takwimu na Utoaji wa taarifa

## Beijing +10 (2005): Kuongeza Umakini katika Kukinga na Kutoa huduma za usaidizi kwa Kina

- **Mafanikio:** Sheria mpya zilizopitishwa, kutambua mahitaji ya huduma jumuishi za kina
- **Changamoto:** utekelezwaji wa sheria usio thabiti, huduma duni kutokana na ufinyu wa rasilimali na kutopatikana kwa huduma , haswa kwa jamii za walio vijijini na zilizopembezoni.
- **Mahitaji muhimu:** utekelezaji kwa kiwango cha juu wa sheria na sera, kuhuisha Ukatili Dhidi ya Wanawake katika mipango ya utekelezaji ya kitaifa, kuboresha upatikanaji wa huduma.

## Beijing +15 (2010): Kuhuisha Ukatili Dhidi ya Wanawake katika Mfumo wa Haki za Binadamu

- **Mafanikio:** Kutambua Ukatili Dhidi ya Wanawake kama suala la haki za binadamu, kuhuisha Ukatili Dhidi ya Wanawake katika sera za maendeleo za kitaifa, kuongeza umakini zaidi kwa tabia zinazochangia Ukatili Dhidi ya Wanawake katika makundi maalum.
- **Changamoto:** utekelezwaji wa sheria usio thabiti, viwango vya ukatili vilivyokidhiri kwa wakimbizi na makabila madogo.

- **Mahitaji muhimu:** Kuwepo na ufadhili mkubwa zaidi kwa ajili ya programu za kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake, kuendeleza utetezi na uwajibikaji juu ya maazimio yaliyotolewa.

### Beijing +20 (2015): Kuhuisha Ukatili Dhidi ya Wanawake katika Mfumo wa Haki za Binadamu

- **Mafanikio:** kuongezeka kwa sheria zinazoshughulikia suala la Ukatili Dhidi ya Wanawake, kutambua tabia zinazochangia ukatili katika makundi maalum.
- **Changamoto:** utekelezaji wa sheria usio thabiti, kiwango kidogo cha ufadhili, kuongezeka kwa unyanyasaji katika mtandao
- **Mahitaji muhimu:** utekelezaji thabiti wa sheria, ulinzi dhidi ya unyanyasaji wa kidijitali na mtandaoni katika mifumo ya kisheria, ongezeko la usaidizi kwa wanawake walio kwenye maeneo yaliyoathiriwa na migogoro ya vita._

### Beijing +25 (2020): Kushughulikia Ukatli katika Muktadha wa Migogoro katika nganzi ya Dunia

- **Mafanikio:** Kutambua uwiano uliopo katika kipindi cha migogoro (kama vile UVIKO-19) na ukatili majumbani, umakini zaidi unahitajika katika kuzuia ukatili mtandaoni na usalama wa kidijitali
- **Changamoto:** Ongezeka la vitendo vya ukatili wakati wa kufungwa kwa shughuli za kawaida katika jamii, huduma duni za usaidizi kwa wahanga wa ukatili wakati wa dharura, ukosefu wa rasilimali & kutokuwepo na utashi wa kisiasa katika utekelezaji wa mikakati ya kutokomeza Ukatii Dhidi ya Wanawake
- **Mahitaji muhimu:** mahitaji ya haraka ya ufadhili katika kuzuia na kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Wanawake na mipango ya dharura, na ulinzi wa wanawake dhidi ya unyanyasaji wa kidijitali.

# Matarajio ya Mbele: Tunatoa wito wa Kuendeleza Utetezi na Kuchukua Hatua za Beijing +30

Beijing +30 inatoa wito wa kutoa ahadi ya maazimia mapya ya kimataifa ya kukomesha ukatili dhidi ya wanawake, kutoa fursa ya kutathmini maendeleo yaliyofikiwa na kutoa maazimio mapya ya kuchukua hatua za kuzuia ukatili na kusaidia waathirika.

Umakini zaidi uhahitajika katika kuzingatia:

- **Uwajibikaji**
    - Katika kuimarisha taratibu za uwajibikaji ili kuhakikisha utekelezaji wa sheria na sera zinazoshughulikia Ukatili Dhidi ya Wanawake kikamilifu.
- **Rasilimali**
    - Kushinikiza uwepo wa ufadhili endelevu haswa wakati ukatili unaendelea kujitokeza katika sura mpya, ikiwemo ya kidijitali na katika muktadha wa baada ya milipuko ya majanga.
- **Maazimio Mapya**
    - Kuwahimiza wadau wa jukwaa la kuchukua hatua la Beijing kuahidi upya kwa kuzingatia mapatano yao ya awali ya kisiasa

Tunapoingia katika awamu ya Beijing +30, tunahitaji kuuliza maswali yafuatayo:

- Ni ahadi zipi zilizotolewa au kuheshimiwa?
- Ni ahadi zipi zimecheleweshwa au zinahitaji kuzingatiwa zaidi?
- Je, mapungufu yatawezaje kushughulikiwa na nani atakayeshughulikia?

Wote tuna jukumu la kufanya ili kuhakikisha uwepo wa dunia ambayo wanawake na wasichana wote wawe huru kusiwe na ukatili katika kizazi hiki kwa kujenga mifumo imara zaidi ya uwajibikaji na inayofikia watu wengi, kuwahimiza wafadhili kufadhili vuguvugu la ufeministi linalofanya kazi ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake, na kufanya utetezi ili kuhakikisha kuwa watunga sera wanatimiza. ahadi zao zilizotolewa kwenye Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing.

**F:** @GBVPreventionNetwork

**I:** @preventgbvnet

**X:** @gbvnet

**E:** info@preventgbvafrica.org

https://preventgbvafrica.org

**Design by:** Samson Mwaka

2024

Building Momentum • Fostering Activism